

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NANE

11 JUNI, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 11 JUNI, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**405. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Changamoto ya fedha za mikopo inayotolewa na Halmashauri za Wilaya kwa Makundi ya Wanawake na Vijana nchini ni urejeshaji hafifu au kutorejeshwa kwa fedha hizo kabisa; kuna Taasisi za fedha hapa nchini zinazotoa mikopo kwa makundi tajwa kwa ufanisi mkubwa na kwa uzoefu wa muda mrefu:-

Je, kwa nini Serikali isipitishe utoaji wa mikopo hiyo kwenye Taasisi hizo zenyenye ufanisi wa muda

mrefu na Wataalam wa kutosha kama WEDAC ili
kuepusha upotevu wa fedha za Serikali na
mikopo kuwafikia walengwa.

**406. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR
(NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya
Rais (TAMISEMI):- Taasisi za Umma na Taasisi
binafsi zimeitikia wito wa Mhe. Rais wa
kutengeneza Madawati kwa ajili ya Shule zetu
nchini:-

Je, Serikali na Mamlaka husika zimejipanga vipi
katika kuhakikisha utunzaji bora wa Madawati
hayo.

**407. MHESHIMIWA SUSAN LIMBWENI KIWANGA
(MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya
Rais (TAMISEMI):- Jimbo la Mlimba lina Vijana
wengi wanaomaliza Elimu ya Msingi, Sekondari
na Vyuo lakini wanashindwa kujajiri kwa kukosa
elimu ya ufundi kutokana na Jimbo hilo kuwa na
Kituo kimoja cha ufundi stadi kilichopo Mchombe
Shule ya Msingi. Hata hivyo Kituo hicho chenye
mahitaji ya Walimu sita kina Walimu wawili
pekee na hakina vifaa. Aidha, Kituo kilichopo

Shule ya Msingi Mpanga hakina walimu wala vifaa:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaboresha Vituo hivyo vya Mchombe na Mpanga kwa kuwapelekea Walimu na vifaa;
- (b) Vijana wachache wanaomaliza Kituo cha Mchombe na kufanya mitihani ya NECTA hawapewi Vyeti; Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu mzuri katika Vituo hivyo ili wawe wanapewa Vyeti ili waweze kuijendeleza katika Vyuo vya Serikali na kupata madaraja;
- (c) Kwa kuwa Mitaala ya Vyuo vingi imepitwa na wakati, Je, Serikali haioni haja ya kuboresha Mitaala ya Vituo hivyo iendane na wakati uliopo kama Vyuo vya VETA.

408. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwepo na malalamiko mengi juu ya Wananchi wanyonge hususan Wanawake Wajane na Yatima kudhulumiwa ardhi hususan maeneo ya Vijijini:-

Je, ni lini Serikali itaweka mikakati ya Kiwilaya ili kuwasaidia Wananchi hao.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

409. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Serikali kuitia Kanuni mbalimbali za Utumishi inatambua Mtumishi na Mke au Mume na Watoto au Wategemezi wanne. Hata hivyo Utumishi wa Umma haumtambui Baba wala Mama hasa linapotokea tatizo la msiba, mara zote huduma za misiba ya Wazazi zimekuwa ni jukumu la Mtumishi mwenyewe:-

Je, ni lini Serikali itawajumuisha Wazazi wa Mtumishi kama wanufaika wa huduma mbalimbali anazopata Mtumishi wa Umma.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

410. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Kwa mujibu wa Ibara ya 141 (2) ya Katiba ya Nchi, deni la Taifa maana yake ni deni lenyewe, faida inayolipwa juu ya deni hilo, fedha zilizowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni hilo polepole, pamoja na ghamra zote zinazoambatana na deni hilo:-

- (a) Je, deni laTaifa hadi Swali hili linapojibwa ni kiasi gani;
- (b) Je, mchanganuo wa fedha zilizowekwa akiba kwa ajili ya kulipa deni hilo ukoje.

WIZARA YA NISHATI:

411. MHESHIMIWA DKT. SHUKURU JUMANNE KAWAMBWA (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kampuni ya utafiti wa Gesi na Mafuta imefanya kazi kubwa ya utafiti wa Mafuta na Gesi katika eneo la Mng'ongo Kijiji cha Fukayosi, Kata ya Fukayosi Wilaya ya Bagamoyo:-

Je, ni nini matokeo ya utafiti huo.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

412. MHESHIMIWA ALEX RAPHAEL GASHAZA (NGARA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Nyakahuwa – Rulenge – Murugarama yenye urefu wa KM 85 imeahidiwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami sambamba na barabara ya

Nyakahuwa – Murusagamba tangu kipindi cha Kwanza cha Uongozi wa Awamu ya Nne lakini mpaka sasa barabara hizo hazijatengenezwa:-

Je, ni lini sasa barabara hizi ambazo ni kichocheo cha maendeleo kwa Tarafa za Murusagamba, Rulenge, Kabanga na Jimbo la Ngara kwa ujumla zitaanza kutengenezwa.

413. MHESHIMIWA PASCHAL YOHANA HAONGA (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Mji wa Mlowo – Mbozi kuelekea Rukwa kuitia Kamsamba imekuwa muhimu katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Songwe, Rukwa na Taifa kwa ujumla:-

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuitengeneza kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

414. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:- Tanzania inayo

Makabila yapatayo 124 ambayo yanaongea lugha tofauti na yanazo mila tofauti ambazo wamekuwa wakiziheshimu tangu enzi za mababu:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaandika lugha za Makabila hayo ili yasiweze kupotea kwenye uso wa Dunia;
- (b) Je, ni lini Serikali itaandika historia ya kila Kabilia nchini ili Vijana wanaokua waweze kujua tamaduni za Makabila yao.

DODOMA
11 JUNI, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE